JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Barabara ya Kilimatinde
Cheyo,
S.L.P. 1020,
45112
TABORA,
Barua Pepe: rbctabora@pccb.go.tz.
TANZANIA.
www.pccb.go.tz

TAARIFA YA UTENDAJI KAZI JULAI 2020 HADI SEPTEMBA 2020

TABORA – OKTOBA 15, 2020

TAKUKURU MKOA WA TABORA YAREJESHA ZAIDI YA SHILINGI BILIONI 1.34 ZA AMCOS NA WAKULIMA

TAKUKURU Mkoa wa Tabora kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Septemba 2020 imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na 11/2007 kama yalivyoainishwa katika kifungu cha 7.

Utekelezaji wa majukumu hayo umefanyika kwa kuendelea kufanyia kazi malengo tuliyojiwekea kwa mwaka wa fedha 2020/2021 katika madawati ya Uchunguzi, Elimu Kwa Umma na Uzuiaji Rushwa.

UCHUNGUZI NA MASHTAKA

Katika kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi Septemba 2020 TAKUKURU Mkoa wa Tabora imepokea jumla ya malalamiko 124 ambayo kati yake, 52 yalikuwa na viashiria vya Rushwa, na 52 hayakuwa na viashiria vya Rushwa kati ya malalamiko yaliyopokelewa, malalamiko 09 yalihamishiwa kwenye idara zingine kwa ufatiliaji zaidi. Pia katika dawati la uchunguzi kazi zifuatazo zilifanyika :

- Majalada ya uchunguzi yaliyokamilika ni kumi na nne (14)

- Tumefungua kesi mpya tano (5) Mahakamani
- Kesi (4) zimetolewa maamuzi na Jamhuri ilishinda kesi (03), kesi (1) Jamhuri ilishindwa
- Mashauri ishirini na tatu (23) yanaendelea mahakamani

ELIMU KWA UMMA

Tumeshirikisha jamii katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kuwaelimisha ili ishiriki kivitendo katika mapambano dhidi ya rushwa. Elimu ilitolewa kwa makundi mbalimbali ikiwemo klabu za wapinga rushwa katika shule za msingi, sekondari, watumishi wa umma na mashirika ya Serikali nayo yalielimishwa kuhusu madhara ya rushwa na namna ambayo wanapaswa kupambana nayo.

Kazi ambazo zimefanyika ni pamoja na:-

- Semina **46**
- Kuimarisha na kufungua vilabu vya wapinga rushwa **122**
- Uandaaji wa makala **6**
- Mikutano ya hadhara na mijadala ya wazi **60**
- Utoaji wa habari na vipindi redioni **06**
- Maonesho yaliyofanyika **02**

UZUIAJI RUSHWA

Dawati la uzuiaji rushwa lina majukumu makuu mawili ambayo ni ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uchambuzi wa mifumo. Majukumu yote haya yana lengo la kuweza kubaini uwepo wa viashiria au vitendo vya rushwa ili kuweza kuchunguza au kushauri mamlaka husika namna bora ya kuziba mianya ya rushwa.

Uchambuzi wa mifumo.

Katika kipindi cha Julai 2020 – Septemba 2020 TAKUKURU Mkoa wa Tabora imefanya chambuzi za mifumo na imefuatilia maazimio mbalimbali yaliyotokana na chambuzi za mifumo zilizofanyika ili kuhakikisha kuwa wadau wanatekeleza

majukumu yao kama yalivyoainishwa katika vikao vya makubaliano. Ufuatiliaji uliofanyika ni pamoja na maazimio katika maeneo yafuatayo:

- Uchambuzi wa mfumo wa ushuru wa huduma (service levy) 07 zimefanyika
- Warsha 02 na ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio 1 umefanyika

Miradi ya maendeleo.

Miradi ya maendeleo katika ujenzi wa miundombinu ya maji yenye thamani ya Sh 85,793,139.11 imefuatiliwa na baadhi yake ilibainika kuwa na dosari na uchunguzi unaendele.

Miradi ya maendeleo kwenye sekta ya elimu yenye thamani ya sh 1,090,249,301.44 ilifuatiliwa na kujiridhisha na ubora wake.

FEDHA ZILIZOOKOLEWA

Kuanzia Julai 2020 hadi Septemba 2020 TAKUKURU Mkoa wa Tabora imefuatilia na kuokoa fedha jumla ya Sh. 1,285,470,347.42 katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:-

- Shs 1,251,566,469.9 ni kiasi kilichookolewa na kurejeshwa kwa wakulima baada ya uchunguzi kubaini wakulima kuuza tumbaku pasipo kulipwa na sehemu ya fedha hizi zilirejeshwa baada ya kufanyiwa ubadhirifu kwenye vyama vya msingi.
- POS Mashine: Sh 20,385,377.52 hizi ni fedha zilizokusanywa lakini hazikuingizwa kwenye akaunti ya serikali.
- Kiasi cha shs 8,018,500/= kiliokolewa katika sekta ya elimu baada ya kubaini kufanyika malipo mara mbili kwenye kazi moja.
- Mikopo yenye riba kubwa (mikopo umiza) shs 2,500,000/= na
- Mwananchi aliyedhulumiwa mshahara wake baada ya kufanya kazi kwenye kampuni ya ujenzi pasipo kulipwa kiasi cha Sh 3,000,000/=

Aidha, kati ya Julai hadi Septemba 2020 TAKUKURU Mkoa wa TABORA ilifanikisha urejeshwaji wa Shs 1,348,675,330.87 kwenye vyama vya msingi AMCOS na wananchi kama iffuatavyo:-

- Vyama vya msingi (AMCOS) 12 katika Wilaya ya Urambo na Vyama vya msingi 11 katika Wilaya ya Kaliua TAKUKURU Mkoa wa Tabora ilifuatilia, hivyo kiasi cha Shs 1,163,717,560.80 toka kampuni ya Magefa Growers Limited kimelipwa kwa AMCOS hizo zikiwa ni deni la kununua tumbaku kwenye wilaya ya Kaliua na Urambo.

- Shilingi 103,446,770.07 zilirejeshwa kwa wakulima wa tumbaku wa chama cha ushirika cha Imalamakoye AMCOS ya Urambo

- Kiasi cha shilingi 16,500,000/= zimerejeshwa Nyota ya Muungano AMCOS zikiwa ni fedha zilizookolewa kwenye malipo ya ujenzi wa ghala wakati ghala halikujengwa

- Shilingi 220,000/= zimerejeshwa kwenye Chama cha Ushirika cha NSENDA AMCOS ya Urambo.

- Kiasi cha Shilingi 38,148,000/= kimeokolewa na kurejeshwa MIBONO AMCOS Wilaya ya Sikonge.

- Kiasi cha shilingi 25,443,000/= kimerejeshwa na chama kikuu cha ushirika WETCU baada ya kukata kimakosa kama gharama ya kusambaza **mifuko 660** ya mbolea ya NPK kwa MTAZAMO AMCOS ya Kaliua msimu wa mwaka 2013/2014.

- Shilingi 1,200,000/= kimerejeshwa kwa mwananchi Kadala Kiteseka Mwigulu wa kijiji cha Ntiliga Mdaka baada ya kuombwa rushwa ya shilingi 1,700,000/= ili asifikishwe polisi kwa madai kuwa alihusika kwenye mauaji ya mke wake.

MIKAKATI TULIYOJIWEKEA KWA KIPINDI CHA OKTOBA 2020 - DISEMBA 2020

TAKUKURU mkoa wa Tabora inaendelea kuweka mkazo katika kufuatilia vitendo vya rushwa kwenye uchaguzi na kuelimisha wananchi kuhusu madhara ya rushwa kwenye Uchaguzi Mkuu wa Madiwani, Wabunge na Rais utakaofanyika Oktoba 28, 2020. Hii ni katika kuhakikisha kuwa wananchi na wagombea hawajihusishi na vitendo vya Rushwa na wanapatikana viongozi wenye maadili.

TAKUKURU mkoa wa Tabora, inatoa rai kwa wananchi wote wa mkoa huu kufuata taratibu na sheria za nchi. Yeyote atakayebainika kujihusha na uvunjifu wa sheria na vitendo vya rushwa kabla, wakati na hata baada ya uchaguzi hatutasita kumchukulia hatua kali za kisheria, kwa kuwa inawezekana tukafanya uchaguzi usiogubikwa na vitendo vya rushwa.

Niwakumbushe wananchi wa Mkoa wa Tabora, tukirubuniwa na wanaogombea nafasi ya uongozi kwa kutupa rushwa nasi tukakubali athari zake ni kubwa sana kwani hatutapata maendeleo stahiki. Hao waliochaguliwa baada ya kutupa rushwa watataka kurudisha fedha walizotumia wakati wa uchaguzi. Tusiwakubalie watununue kwa kutupa vizawadi kwani vinadhalilisha utu wetu.

Wananchi wa Mkoa wa Tabora tukumbuke***, KURA YAKO NI MAENDELEO YAKO: USIPOKEE WALA KUTOA RUSHWA ILI UCHAGUE AU KUCHAGULIWA***

Asanteni sana

Imetolewa na:

Musa Chaulo
MKUU WA TAKUKURU (M) TABORA